

*Huduma ya
Kikristo ya
Tony Alamo*

Jarida la Dunia

YERUSALEMU MPYA

Makanisa Ulimwenguni Kote

Mchungaji Tony Alamo

Taifa la Kikristo la Alamo

Toleo 13200

ASKARI WA JANGWANI

na
Tony Alamo



Picha ya Mchungaji Tony Alamo
1986

Malaika wa BWANA akasema na Filipo, akamwambia, "Ondoka ukaende upande wa kusini hata njia ile itelemkayo kutoka Yerusalemu kwenda Gaza; nayo ni jangwa" (Matendo 8:26).

Mhubiri Filipo akaelekea Samaria, Akiwa huko uvuvio ukatokea, uvuvio huo uliambatana na nguvu ya miujiza. Wagonjwa waliponywa, pepo walikemewa, utukufu wa BWANA ukaonekana, na mji mzima ulitekwa na mahubiri ya Filipo. Filipo alikuwa kwenye upeo wa huduma ya kimitume na MUNGU alitembea kupitia kwake. Basi usiku mmoja MALAIKA wa BWANA aliongea naye na kumwambia, "Amka ujitarishe, uache kazi unayofanya na ushuke kwenda Gaza jangwani." Nadhani Filipo alijiuliza maswali mengi moyoni mwake kulingana na maelekezo aliopewa, kwamba aache kazi ya utume aliyokuwa akiifanya. Kuacha kazi ya MUNGU? Kuacha kazi njema ya kutangaza nguvu za MUNGU na kushuka jangwani? Hakuna maji wala chombo cha kurekebisha hali ya hewa jangwani. Hakuna mikahawa ya McDonald au Colonel Sanders. BWANA sipendi jangwa; napenda kubaki hapa katika uvuvio. Uvu-

vio unanihitaji. Nguvu za MUNGU zinatawala hapa, uvuvio unaendelea, roho zinaokolewa, Ninahitajika hapa!

Basi, Filipo akaanza safari yake kupitia Yerusalemu katika njia kuu iendayo pembezoni mwa pwani ya Mediterania na Afrika ya Kaskazini. Wakati alipokuwa akitembea barabarani alikuwa akisali. "Naam sasa, BWANA nimefika hapa. WATAKA nifanye nini?" Na alipotazama akaona magari ya kifahari ya kipindi hicho – Tajiri akiwa kwenye gari la farasi, akiwa amevalia mavazi ya kifalme. Alikuwa akisoma chuo cha nabii Isaya, baada ya kumwona Filipo, akaamuru gari kusimama, na kumualika Filipo karibu yake. Basi Filipo alimsogelea yule tajiri, akamkuta anasoma chuo cha nabii Isaya; akanena, "Je! Yanakuelea haya unayosoma?" (Alikuwa akisoma sura ya 53 ya chuo cha Isaya iliyomwongelea BWANA YESU KRISTO.) Akajibu, "Nitawezaje kuelewa mtu asipo niongoza?"

MUNGU alimtuma Filipo kumweleza yule mtu habari ya maandiko yale. Basi mtu yule aliamini, akaokoka, na kubatizwa, yote yalifanyika siku iyo hiyo. Historia inatuambia kuwa mtu huyu alikuwa

kwenye mamlaka ya juu, katika hazina ya Ethiopia, aliyerudi Ethiopia akaeneza NENO la MUNGU kwa watu wa mahali pale na kuanzisha Kanisa (Kanisa ambalo mizizi yake ipo mpaka leo, na hii ni kwa sababu Filipo alikuwa mtii wa NENO la MUNGU na kushuka jangwani).¹

Watu wengi wa MUNGU wamekuwa wakitumwa jangwani.² Hili ni swala ambalo kila mmoja wetu angependa kuepukana nalo kwa namna yoyote. Hatujisikii vizuri pale MUNGU anapoingilia ratiba zetu na kusema "Nataka ushuke jangwani." Lakini katika maisha yoyote ambayo MUNGU anatumia lazima kuwe na uzoefu wa jangwa. Katika uzoefu wa Filipo, MUNGU alimuhudumia; alichukuliwa katika ROHO na kutolewa jangwani hata pembezoni mwa bahari kwa nguvu za kimiujiza za MUNGU.

Uzoefu wa jangwa ni lazima katika maisha ya watu wa kweli wa MUNGU.³ Mungu hachagui kusanifisha vyombo vyake safi kwenye mji, bali jangwani. Unaweza kumtambua mtu aliyeko jangwani kwa sababu mara kadhaa utamsikia akisema, "Nahisi ukame, nazona mbingu kama

(Inaendelea ukurasa wa 2)

¹ Mdo. 8:26-40 ² Mwa. 6:14-22, 12:1-4, 15:1-8, 22:1-18, 1 Fal. 17:1-7, 19:2-4, Yoh. 4:5-8, Mat. 4:1, Rum. 4:16-21, Ebr. 11:7-19 ³ Zab. 34:18

ASKARI WA JANGWANI

(Inaendelea kutoka ukurasa wa 1)

chuma kwangu, na sielewi kwa nini haya yote yananitokea mimi.” MUNGU anaku-pa uzoefu wa kuishi jangwani. Tunapenda kufanya huduma za kiroho, kujitolea na kusaidia, ni vema. Tunapenda sana kuwa kati ya watu wengi. Tunapenda kuendelea, Lakini MUNGU anatuambia, “Kijana (au binti), nataka uje pembedi. Nataka nikutoe kwenye halaiki ya watu. Nataka nikutenge. Nataka nikuweke peke yako, hapa nje chini ya nyota kwenye sehemu ya upweke, mahali ambapo naweza kuongea nawe. Nataka Kuchomelea NENO LANGU ndani ya roho yako ya milele.⁴ Nataka kuweka ujumbe WANGU kinywani mwako.⁵ Nataka kuingia ndani vilindini mwa nafsi yako, Nataka nikutumie.⁶ Na hili ni swala ambalo mara nyingi hatujajiandaa kufanya. Tunalamika, “Sipendi sehemu pweke. Ningependa kuzungukwa na watu. Ningependa watu wajue ninachokipitia. Ningependa watu wanionee huruma. Ningependa watu wanielewe. Ningependa faraja ya watu wengine.” Lakini MUNGU anasema, “nitakuweka kwenye jangwa, na kama unanipenda MIMI na kuamini NENO langu, utakwenda jangwani. Nakupeleka huko ili nikutane na wewe, peke yako, jangwani.”

Hebu tuzungumze kuhusu jangwa. Namshukuru MUNGU kwamba viro vijito vya maji. Namshukuru MUNGU kwa vilele vya milima. Lakini pia namshukuru MUNGU kuwa katika maisha ya kila mwananaume na mwanamke anayetitia Mkristo, kuna ahadi ya mwisho kwetu. Kila mmoja atakaye kuja na ujumbe uchomao nafsi, na kila nabii aliye na ujasiri wa kusimama mbele ya taifa na hata ulimwengu, basi huyo ni mtu ambaye MUNGU amempeleka kwenye sehemu pweke – jangwani – sehemu pweke – sehemu ya kiza nene – sehemu isiyo nyevu – hiyo ni sehemu ambayo MUNGU anaongea na kuvunja na kuunda na kutengeneza na kujenga.⁷ Basi MUNGU anaweza kumtuma mtu huyo kutoka kwenye jangwa na maji yapeanayo uhai na ujumbe wa wokovu wa mbinguni.

MUNGU alipomuita Musa, alikuwa na umri wa miaka minane. Alimwezesha Musa kupokea Elimu na kuishi kama mwana wa mfalme.⁸ Kwa muda wa miaka arobaini amekuwa akisubiriwa na kulishwa. Alioga kwenye maji ya vijito vya mto Nile huku watumishi wake wakimsibiri. Alivaa nguo nadhifu na kusherehekea vyakula vya kifalme kwenye meza ya Farao akijifunza utamaduni wa Wamisri. Siku moja, MUNGU akamwambia Musa, “Sehemu ya kwanza ya elimu yako imekwisha, na sasa nina mkutano muhimu sana nawe.” MUNGU akamchukua hadi sehemu ya nyuma ya jangwa.⁹ Kwa miaka Arobaini mingine alitembea jangwani ngozi yake ikaungua kwa jua, na macho yake yakawamekundu kwa sababu ya changarawe, mpaka MUNGU alipotimiza kazi yake ya kuifanya roho ya Musa kulizoea jangwa.¹⁰ Sasa MUNGU alikuwa tayari kukutana na Musa. Maisha yake yaligawanya katika sehemu tatu za miaka arobaini kila moja; Miaka arobaini Misri, Miaka arobaini jangwani, na miaka arobaini katika hukumu; na alipewa sheria kwa Israeli na kwa dunia.

Musa alikuta kichaka kiwakacho kwenye sehemu ya nyuma ya njangwa.¹¹ Alisikia sauti ya BWANA, akatii, akarudi na moto wa unabii na utukufu wa MUNGU katika moyo wake.¹² Aliongoza kati ya Waisraeli milioni mbili hadi tatu toka utumwani, akifanya ishara kubwa na maajabu na miujiza – kwa sababu alikutana na MUNGU jangwani.¹³

Ikiwa unawaendea watu wa MUNGU kwa ishara na maajabu na miujiza, na kubeba fimbo itakayoleta ukombozi, basi kuna kichaka cha MUNGU kinachowaka katika jangwa lake kwa ajili yako, kitu ambacho ni lazima ukutane nacho kwanza. Usidhani kwamba yupo mtu atakayekuita kutoka katika umati kanisani na kukuweke mikono na kukugawia huduma ambayo itawatoa wanaume na wanawake kwenye upofu na utumwa. Usidhani kuwa utaenda shule ya Biblia na kutunkuwa Shahada itakayokuwezesha kuwaokea watu. Kama unataka kuwatoa watu kwenye utumwa wa Misri, basi unahitaji kuonana na MUNGU kwenye sehemu ya

nyuma ya jangwa. MUNGU atakuondolea raha zote, atakuondolea starehe zote, atakuchukulia vitu vyote ulivyopendezwa navyo, atakupeleka mbali na watu, na katika ROHO WAKE, atakupeleka mahali ambapo utakuwa wewe na MUNGU peke yake. Kila nabii wa kweli wa MUNGU, kila askari wa BWANA, na yejote anayetarajia kutimiza malengo ya MUNGU ni lazima akutane na Muumba wake kwenye sehemu ya nyuma ya jangwa.

Yusufu, njoo na utoe ushuhuda. “Mimi ni mtoto wa kumi na moja kwa baba yangu.¹⁴ Nimekuwa na ndoto na maono ya kiroho,¹⁵ na nilijua nina mkutano na MUNGU; lakini nilikuwa nikiishi katika sehemu ya upweke. Watoto wa baba yangu, kaka zangu, walnidharau.¹⁶ Niliishi kama mtu aliyetelekezwa kwenye nyumba ya baba yangu.¹⁷ Mimi ndiye nilitupwa kizuijini na kwenye huzuni ya jela.”¹⁸ Yusufu, unawezaje kuishi kama mtoto wa mfalme katika nchi? Je! Unao uzoefu wa jangwani? “Hakika, nilihitimu mahitaji ya kumfanya MUNGU kazi nikiwa kwenye gereza la Farao.” Wapi ulijifunza usawa na kusamehe? Ulijifunzia wapi huruma dhdidi ya wanadamu wengine? “Nilijifunza wakati nikilia kwenye dimbwi la upweke ndani ya gereza la Farao. Hapo ndipo niliopoifunza huruma ya MUNGU.”

Yohana, unawezaje kuwa na lugha ya kushawishi kiasi hicho? Yohana, unawezaje kushawishi halaiki yote hii ya watu kufanya toba? Yohana, ni jinsi gani umepata moto na nguvu hizi na shauku ya namna hii maishani mwako, kiasi cha kushawishi taifa kwa mahubiri yako dhidi ya dhambi? “Niliondoka nyumbani kwa baba yangu nikiwa kijana mdogo nilienda kuitikia wito wa ROHO MTAKATIFU, na kuishi jangwani.¹⁹ Nilivaa mkanda wa ngozi, na nilikula asali na nzige,²⁰ na nikakutana na BWANA MUNGU kwenye jangwa. NENO la MUNGU likaniingia moyoni mwangu, na nikatoka jangwani nikiwa na bidii na utukufu wa MUNGU moyoni mwangu. Ni kipindi hicho pekee niliweza kuhubiri kwa watu juu ya toba na kuwafanya watu wamwabudu.

Baada ya Paulo kubadilishwa kwenye njia ya Dameski, alimuhubiri KRISTO

4 Mit. 3:3, Yer. 31:33, Ebr. 8:10, 10:16 5 Zab. 81:10, Yer. 20:9, Mat. 10:19-20, 13:23, Mk. 16:15, 1 Kor. 1:17-18, 21, 2 Tim. 3:16-17, 4:2 6 Rum. 12:1, 2 Kor. 5:18-20, 9:8, Flp. 1:6, Ebr. 4:10-16, 13:21 7 Rum. 5:3-5, 2 Kor. 12:9 8 Kut. 2:1-10, Mdo. 7:22 9 Mwa. 2:15-22, Ebr. 11:24-27 10 Mdo. 7:29-34 11 Kut. 3:2-10 13 Kut 3:10-22, Mdo. 7:34-36 13 Kut. 4:1-9, 28, 6:13-37, Kur. 7-14 14 Mwa. 30:22-24, 37:2-3 15 Mwa. 37:5-10 16 Mwa. 37:4-11, 17-20, Mdo. 7:9 17 Mwa. 37:4-11 18 Mwa. 39:6-20, Zab. 105:18 19 Mat. 3:1, Lk. 1:13-17, 67-80 20 Mat. 3:4

kwa muda.²¹ Kisha akaenda katika jangwa la Uarabuni kwa miaka miwili.²² Maandiko hayatuambii chochote kuhusu miaka hii, lakini alipotelea jangwani kwa muda wa miaka miwili na kuishi maisha ya upweke katika sehemu iliyojitenga. Tangu hapo alirudi akiwa mtume kamili wa MUNGU.

Na hata WEWE, BWANA YESU; WEWE uliyesimikwa kabla ya kuwekwa kwa misingi ya ulimwengu kuleta wokovu wa uzima wa milele kwa ulimwengu uliopotea na mauti.²³ EWE YESU – uliye BWANA unaenda wapi? Je unakwenda katika hekalu la Yerusalem kujitangaza kama MASIHI? “Hapana, nimesukumwa na ROHO kwenda nyikani kwa siku arabolini.”²⁴ Na ndani ya siku hizo za kufunga na kuomba, alimthibitishia Shetani nguvu ya NENO TAKATIFU la MUNGU na kutoka jangwani, akiwa amejawa neema na kweli, kutimiza kazi ile iliyomleta kutoka mbinguni.²⁵ Naam, hata YESU MFALME alipitia wakati wake wa jangwani, tena mara nyingi zaidi.

Kila mwanaume na mwanamke ambaye MUNGU amemwekea mikono na kumwita katika huduma ni lazima apitie jangwani kwanza. Ninazungumzia sehemu ya upweke katika maisha yako ya kiroho ambapo MUNGU anakutenga na wengine, kipindi ambacho watu hawakuelewi, hicho ndicho kipindi cha kutumiwa na MUNGU. MUNGU anasema “sitamtuma mtu akuombee ama kukuwekea mikono. Itakubidi ujiombee wewe binafsi.”²⁶ Utaonana na MWENYEZI MUNGU uso kwa uso. MUNGU atakupeleka jangwani ambapo aidha utaelewa mwenendo wako na MUNGU au utakufa. Utamwangukia MUNGU na kulia kwa uchungu mpaka utakapopata kibali mbele za MUNGU. Utatengeneza mahusiano mapya na MUNGU. Na hutajali MUNGU atapokwambia nenda Ninawi, kwa sababu utakuwa kwenye kiti cha enzi cha MUNGU, na utukufu WAKE utakuwa usoni mwako bila kupunguka. Nazungumzia kuhusu mahali ambapo MUNGU atakuelekeza, na utapokea maelekezo YAKE. Sehemu ambayo hutapata faraja ya mwanadamu, mahali ambapo hakuna ye yote anayelewa unachofanya.

Unafikiri Daudi alipitia hali gani wakati akiwa na watu mia sita na hakuna aliywewelewa? Alisema “Roho yangu ina kiu ya uhai; MUNGU, umekwenda wapi? Siwezi kuhisi uwepo wako. Nafsi yangu ina kiu ya MUNGU aliye hai.”²⁷ Daudi alikuwa mahali ambapo MUNGU hakuja kuzungumza naye, na akasimamia NENO la MUNGU ambalo lilikua ndani yake. Alilazimika kuwa na imani katika wema na rehema za BWANA, ili MUNGU kwa namna fulani ampitishe kwenye majaribu haya na jangwa la kiroho.²⁸

MUNGU anajaribu kuwakuza watu waume na wake. Unasema, “MUNGU aliniita kutabiri.” Oh! Alikutuma? Kweli? Kwanza ngoja nione changarawe kwenye viatu vyako. Manabii wa kale walipokuja na NENO la BWANA, wengine walipigwa mawe, wengine walifungwa jela, wengine walitengwa na kuteswa na hata kuuawa.²⁹ Na wewe, unapopata mateso kidogo, unailia na kusema, “Nitarudi nyuma” lakini kama UTAMRUHUSU na kudumu katika ROHO WAKE, MUNGU atakusani-fisha katika jangwa hilo na kukukuza.

Utakuja wakati kwenye maisha yako ambapo MUNGU atawafungia watu nje na kujifungia ndani akiwa na wewe, nawe utalia, “MUNGU hakuna anayenielewa.” MUNGU atakujibu, “sitaki wakuelewe. Unachotafuta ni bega la kuegemea, nami nataka uegemee bega langu.” Baadhi yenu mpo jangwani hivi sasa, wengine ndio mnatoka jangwani. Mmekuwa na MUNGU, mnaongea na MUNGU, na MUNGU anaongea nanyi. Mmekidhi vigezo vya MUNGU. Mmeipata sehemu ile ya MUNGU ambapo hamteter-eki wala kutikisika. Hampepesuki katika maisha yenu ya Ukristo. Mmekutana na MUNGU uso kwa uso na kwa uhalisi. Mmejifunza masomo ya jangwani vizuri. Mnajua namna ya kusali, mnajua namna ya kutunza ahadi ZAKE. Mnajitambua, na mnamtambua MUNGU, hamhitaji uthibitisho wa binadamu, kwa sababu mmesikia kutoka kwa MUNGU MWE-NYEWE. Hamsikilizi kutoka kwa mwanadamu, bali mnaongea na MUNGU moja kwa moja, naye anaongea nanyi.

“Ondoka na uende jangwani, nina jambo nawe huko jangwani: Mashaka, masikitiko, maumivu ya moyo, mabadi-liko.”³⁰ Unaweza ukawa jangwani kimwili, au ukawa kimawazo, au ukawa huko kiroho. Lakini MUNGU anashughulika na moyo wako huko jangwani.

Kwa nini, Filipo, kwa nini unakwenda jangwani? “Kwa sababu kuna mtu huko atakaye uleta Ufalme na hata taifa kwa MUNGU.” MUNGU hakuweki sehemu ya shida kwa sababu hajafurahishwa nawe. MUNGU anaruhusu tu wale bora zaidi kuteseka. Mateso hayapo kwa ajili ya watu wasio na msimamo dhabiti ndani yake, kwa sababu MUNGU hatajisumbua kusaga kitu kingine bali ngano iliyo safi.³¹

Utajiuliza, “Kwa nini imekuwa rahisi sana kwa wengine, na ngumu sana kwan-gu?” Imekuwa rahisi kwa sababu MUNGU hakuwataka wasimame kama mti wa mwaloni. “Kwa nini Fulani ana mali nydingi?” Kwa sababu hivyo ndivyo MUNGU alivyowapatia. MUNGU hana imani nao katika mateso. Hawezi kuwaweka kwenye moto kwa sababu wataungua. MUNGU hapotezi tanuru lake la mate-so. Kama huna dhahabu rohoni mwako, MUNGU hatapoteza tanuru lake kwa ajili yako. Kama hauna kitu ndani yako kinacholeta maisha matakatifu, MUNGU hatakuletea majaribu wala dhiki. Majaribu na dhiki ni kwa watakatifu wa MUNGU waliobeba NENO LAKE. Beji ya mafanikio ya ukristo ni pale mateso ambayo yalimjia YESU, yanapokujia wewe.

Kila mmoja anapenda kubembelezwa na kusikia watu wakinena yaliyo mema kumhusu yeye. Wang’aa kama taa ya neon yenyenye mwanga mkali. Wanataka watu wawapende na kuwawazia mema. Hawataki kusikia watu wakisema, “Usimkaribie huyo. Ni mzushi; yupo kwenye mafundisho yasiyo sahihi.” Lakini MUNGU anasema nini... “Kuwa makini mwanangu, wakati watu wanapoongea mazuri kuhusu. Hiyo siyo beji ya mafanikio. Haupo kwenye rekodi ya MUNGU ya tabia nzuri ikiwa kila mtu ananena vema kuhusu. Lakini wanapokuongelea uba-

(Inaendelea ukurasa wa 4)

²¹ Mdo. 9:3-22 ²² Gal. 1:17 ²³ Mat. 13:35, Yoh. 17:24, Ebr. 5:8-9, 9:24-28, 1 Pet. 1:18-21 ²⁴ Mat. 4:1-2 ²⁵ Mat. 4:2-11, Mk. 1:12-13, Lk. 4:1-14, Yoh. 1:14 ²⁶ Mat. 6:6, Lk. 18:1-8, Efe. 6:18, Flp. 4:6, Kol. 4:2, 1 Thes. 5:17, 1 Tim. 2:8, Ebr. 4:16, 11:6, 1 Yoh. 3:22, 5:14-16, Yud. 20-21 ²⁷ Zab. 42:2, 63:1, 143:6 ²⁸ 1 Sam. 30:6 ²⁹ Mat. 5:10-12, 10:16-18, 21-28, 20:18-19, 23:23-39, 24:8-10, 26:1-4, 47-54, 57-68, Lk. 21:12-19, Yoh. 15:18-19, 16:1-2, Mdo. 6:7-15, 7:51-60, Rum. 8:35-37, 1 Kor. 4:9-13, 2 Kor. 4:8-12, 11:23-26, Gal. 4:28-29, Ebr. 11:32-38, Yak. 5:6, 1 Yoh. 3:1, 13, Ufu. 2:10, 69-11, 7:13-17, 11:3-12 ³⁰ 2 Kor. 4:8-11, Yak. 1:2-3 ³¹ Mat. 3:12, 13:3-9, 18-30, 47-50, 21:44, 1 Pet. 1:6-7, Ufu. 3:18-19

ASKARI WA JANGWANI

(Inaendelea kutoka ukurasa wa 3)

ya na kukutesa na kusema mambo mabaya kwa jina langu kinyume na ukweli, basi furahi na endelea kuishi kwa furaha kwani malipo yako yapo mbinguni.³² Hivyo basi, inapaswa kuwa kama muziki masikioni mwako pale watu wanapoonagea mabaya kuhusu wewe kwa sababu ya jina la YESU.

MUNGU anawatafuta akina Musa na akina Yohana mbatizaji, na akina Yusufu na Debora na Samueli, kwa sababu ulimwengu upo kizani na unahitaji nuru ya uhai. Anahitaji watu waliokwenda nyikani na kukutana naye katika hizo sehemu za siri, katika nyakati pweke, masaa ya maumivu ya moyo, wakati ambaao hauwezi kulala na unahitaji kuomba, mahali anakopajua MUNGU pekee, saa ambazo unyevu ni machozi yanayo bubujika kama mto kutoka machoni mwako ukimlilia MUNGU, "MUNGU, nипитиshe kwenye jaribio hili, nисайди nione siku nyingine, usiniache nianguke, MUNGU, nijalie nguvu, nguvu ya ndani, nipate kusimama upya KATIKA ROHO wako. Katikati ya kilio, mahangaiko na uchungu, MUNGU nijalie nguvu ya kusamehe wakati huu. Usikubali haya maumivu ya-sizidi nikashindwa kusamehe. Nisafishe kwenye damu yako tukufu na unijaze kwa ROHO WAKO." Umepata uchungu usiku kucha hadi kuona juu likichomoza

bila kulala usiku kucha na kitanda kilicho kinyevu kwa sababu ya machozi na jasho, baada ya kupigana na MUNGU ili kuku-tana NAYE na kutokea ukiwa umebadilishwa, kwa sababu MUNGU alisema siku moja "nenda jangwani."

MUNGU huchagua mashuhuda WAKE, kisha kuwafunza jangwani. MUNGU huwapata watu WAKE kwenye haya Majangwa yakukatisha tamaa. Wakati tabia zako zinapopakwa matope na watu kusema maneno ya uchungu na yasiyo haki kukuhusu wewe. Huoni jinsi MUNGU mwenye haki ANGETAZAMA tu wakati unateswa, lakini alisema, "Nakuila ili uende ukapate uzoefu wa jangwani," umeomba, na kuomba, mpaka ukaishiwa vya kuomba, na hata maombi yako yamekuwa Jangwa. Moyo wako un-aumia sana kiasi cha kukaa kanisani na kulia. Huwezi kumwona MUNGU katika nyimbo. Huwezi kumwona MUNGU kwa kucheza. Huwezi kumwona MUNGU katika ibada. Umeishiwa na kila kitu. Ume-fanya kila jema unalolijua, umetoa fungu la kumi na kuamini NENO la MUNGU. Unaangalia salio lako la Benki na kuona una madeni kuliko mapato. Umeeneza NENO la MUNGU kwa watu na kuwa mtoaji kadiri ya uwezo wako, umeonye-sha upendo kwa watu, na malipo yako yamekuwa ni maneno makali ya kejeli. Uko kwenye jangwa. Lakini hapo ndipo MUNGU anapokuja, atachoma yote yaliyo rohoni mwako na ambayo yangekuwa mabaya kwako. MALAIKA wa BWANA (BWANA MWENYEWE) anakuja ku-

zungumza nawe nyikani katika kichaka kiwakacho, Na kusema "unaweza kwen-da sasa. Unayo maneno ya uzima wa milele kwa watu WANGU. Unalo neno la tumaini, neno la wokovu." Hapo ndipo utakapoanza kuwa na shukrani za milele kwa MUNGU kwa kukushughulikia, na unajenga Madhabahu jangwani kwa ajili YAKE. Hutasahau kamwe sehemu am-bayo wewe na MUNGU mlionana ana kwa ana. Utaelewa ni nini maana ya ku-ongozwa na ROHO wa MUNGU kwa ukamilifu na Maji ya Uzima ulyopata yatabadilisha Jangwa kuwa Bustani yenyе mazao mengi. Haya yote ni kwa sababu ya Utii kwa MUNGU ukiwa katika jangwa.

MUNGU anasema "Nataka kutembe-lea watu WANGU. Kilio cha wanadamu kimekuja KWANGU na sina mtu wa-kumtuma. Sitamtuma Nabii asiye tarayi. Sitamtuma muhubiri asiyeongozwa na ROHO. Sitamtuma mtu kuhubiri toba ambaye yeye mwenyewe hajatubu. Sita-tuma mtu asiyeptitia jangwani"

Kisha unaweza kusema, "MUNGU, sasa ninaelewa kuwa kila kitu kipo kama kilivyo, na sasa ninaelewa kwa nini ULYAACHA haya mambo yanitokee na hukutuma hata Mvua jangwani, mahali penye upweke, hali ya kukata tamaa, ku-kataliwa, kukosa, na kutoleweka, kwani ni WEWE ulyienipeleka pale.

Mwanzo hukuelewa; ukasema, "Kwa nini, nimefanya nini? Nimekosea wapi MUNGU? Kwa nini MUNGU hanifun-gulii mlango? Kwa nini nipo kwenye hali

(Inaendelea ukurasa wa 8)

32 Mat. 5:11-12, Lk. 6:20-23, 2 Kor. 5:1, 1 Thes. 4:14-18, Ebr. 4:9, 11:16, Ufu. 22:12-14

Pakistan

Ndugu katika Kristo, Tony Alamo

Salamu katika jina la Yesu, nataka kuwashirikisha katika taarifa kuhusu mkoa wa Peshwir.

Agosti 12, 2011, Nikiwa narudi Nyumbani, muda huo nikakutana na Muhammad D.P alikuwa ni dereva wa magari ya mizigo. Gari lake lilikuwa bovu, nikamwuliza kama naweza kumsaidia! Akanijibu, "ahsante kaka". Lakin ni nikamwuliza tena, "kama hautajali naomba nikuombee katika wakati wako mgumu na ni kushirikishe katika ujumbe wa Mchungaji Tony Alamo kutoka Marekani". Akakubali ombi langu. Anaishi katika mji wa magaidi mahali ambapo jeshi la NATO linapambana hivi sasa.

Hivi leo, alinipigia simu. Ndugu, unaweza ukani-

mia nakala nyingi zaidi kwa sababu nasambaza ujumbe huu kwa wakazi wa mkoa ule na naona mabadiliko zaidi hapa. Hii ni njia bora kubadilisha akili za magaidi. Kupitia utafiti wangu nimegundua kuwa kuna 75% ya magai-di eneo hili. Kupitia ujumbe huu tunaweza kubadilisha roho nyingi zaidi duniani kote. Ujumbe wako umekuwa wa msaada kwangu na familia yangu. Nimefurahishwa sana na hili.

Ningependa kuomba usali kwa ajili ya D.P ili afani-kiwe katika maamuzi yake ya kumchagua Kristo.

Katika Kristo,
Pastor R. B.

Albuquerque na Santa Fe, New Mexico

Ni dhahiri, New Mexico imekuwa sehemu nzuri ya kutembelea mwisho wa juma mahali ambapo mimi na ndugu zangu tunakwenda. Watu huchukua nakala mbili za maandiko ili waweze kumpa mtu yeyote wanayefahamu. Na kwa kuva mashati yetu ya Alamo Christian Ministry tumekuwa tukitoa ushuhuda mpaka kwenye migahawa.

Katika moja ya maeneo ya kuegeshea magari, mwanamke mmoja aliona jarida tuliloweka kwenye gari lake. Alipokuwa akisoma, alianza kutabasamu na kukandamiza jarida hilo kifiani mwake na kuwaonyesha wenzake alio-kuwa nao. Hapo ndipo Mungu anapotuhitaji mwisho wa juma hili. Ametuweka pale tunapohitajika. Hili peke yake lilikuwa ni Baraka, na kuona kuwa hawa watu wanapenda ujumbe wa dini na kuona roho zinazookolewa.

Kwa Mchungaji na rafiki yangu.

Ndiyo nimemaliza kusoma ujumbe wako "Askari wa Jangwa" nilikua naangalia baadhi ya nakala za ujumbe wako. Ahsante, ahsante, ahsante, ahsante!!! Nakushukuru kwa kutushirikisha mimi na ulimwengu mzima katika hilo Mungu alilokupatia.

Mara nyingi katika miaka iliyopita nilichukulia uzoefu wangu wa maisha ya Ukristo kama uzoefu wa 'Jangwa.' Kwa wakati huo sikuelewa kwa nini Mungu anaruhusu baadhi ya vitu kunitokea. Ni baada ya kuwa katika sehemu pweke na Mungu, ndipo Mungu akanipatia ufahamu.

Baada ya watoto wangu kuchukuliwa, nilikua kwenye jangwa kwa mara nyingine. Sikulala, sikujisikia kula, watu hawakuweza kunifaraji, sikusikia chochote kutoka kwa Mungu, nilitaka kufa tu, nilikuwa namilia Mungu, nilikuwa nikilia sana usiku wa manane, Neno la Mungu ndilo lililonifanya nisiteketee kabisa, Roho Mtakatifu wa Mungu, na Nguvu zake. Wakati nimeacha kulia na nilihitaji kulla, nilikuwa na wasiwasi kuhusu watoto wangu na kadhalika, na nilipoamka faraja yangu ilikuwa ni Neno la Mungu.

El Salvador

Mchungaji kutoka El Salvador, ambaye alipokea nakala ya "Kamwe Usizimie" katika lugha ya kihispaniola alitupigia kutoa ushuhuda. Alipenda ujumbe na alitaka kupata ujumbe zaidi na Biblia kwa lugha ya kihispaniola. Alisema kuwa Bwana alimwambia Tony atatoka gerezani siku za hivi karibuni. Kwamba Bwana alimpeleka pale ili kuhubiri neno kwa watu mle ndani, na baada ya kazi yake kumilikia, atatoka. Alimuombea Tony na huduma kuititia kwenye simu, na akasema kuwa Bwana anataka tumuite yeye, Yupo nasi, tumilie yeye bila kuchoka kwa ushindi, ukombozi na wokovu wa roho. Alisema Bwana alimwambia ana ufunuo ambaao angependa auonyeshe kuititia sisi, na hatuwezi kuzimia, lazima tuendelee kuamini kuwa yeye ni Mungu, na ana uwezo wa kufanya makubwa zaidi ya tunayoomba au kufikiri. Ufalme wa Mungu ni ushindi. Tuendelee na sala.

Othelia Carabia de Campo
San Salvador, El Salvador

Arkansas

Hatimaye, nahisi Mungu alichoshwa na 'kulia' kwangu, siku moja ni-kiwa nalia na kusali, Mungu alisema moyoni mwangu, Aliongea na moyo wangu na kunikemea. Aliniambia kuwa anaelewa jinsi ninavyojisikia; na ameshapitia yote, ya kwamba si tu alitengana na Mtoto wake, bali alimtoa mtoto wake afe kwa ajili ya wato-to wangu na watoto wa watu wen-gine. Alinitaka nimuachie jambo hili mikononi mwake na niwe na imani kwamba atatenda. Nilijisikia nafuu sana. Nimekuwa nikiwaza sana kuhusu kinachonitokea kuliko kumua-chia Mungu. Inaonekana rahisi sana, mambo uliyonifundisha kwa miaka mingi, lakini hapa nilikuwa kwenye jaribu kweli. Sisemi ilikua rahisi ku-pitia katika jaribio hili ila baada ya Mungu kunikemea nilijisikia amani sana. Sasa niliweza kuelekeza malengo yangu kwa Bwana na kugundua kuwa Mungu anaweza yote wakati wote. Mungu aliacha haya yote yanitokee ili tu Utukufu wake ukamilike.

Katika ujumbe wako ulisema "Mungu atakupeleka kwenye jangwa

ambapo aidha utaimarika au utaku-fa... Mungu anajaribu kuwajenga wa-naume na wanawake. Mungu hapotezi tanuru lake la dhiki. Kama hauna dhahabu rohoni mwako, Mungu hatapoteza tanuru kwako. Kama huna kitu kilicho na maisha matakatifu, Mungu hatakutia majaribuni."

Sisemi kwamba hakutakuwa na majaribu zaidi, bali tu hili jaribu likikuwa kubwa zaidi na Mungu alini-toa kwenye lile jaribu. Nina uhakika kwamba kuna kukua na kukomaa kunaokuja, lakini nilitaka kushukuru kwa miaka uliyotumia 'kutoa nafsi ndani yangu' na kunifundisha kuishi kikristo, ile miaka haikuwa ya bure. Bado napambana pambano zuri. Nakushukuru kwa mfano wako wa hai-jalishi nini umepokea au kupoteza ungali umesimama imara!

Nashukuru kwa ujumbe wako na uvumilivu wako!

Binti yako katika Kristo,
Becky Avila

P.S. Mwaka wa77 wenyewe furaha, Mungu akubariki, tutaonana siku si nyingi!!!

Kalifornia

Ndugu Mchungaji Tony,

Daima u katika mioyo yetu na sala zetu. "Ni nani atakaye tutenga na upendo wa Kristo?" (Warumi 8:35-39). Hii ni Huduma ya Mungu inayopingwa na wapinga kristo, tuhuma kwamba wewe, Mchungaji Tony, unatawala akili zetu ni mbinu nyingine ya shetani kujaribu kurarua uhalali wa nguvu za Roho Mtakatifu zinazo tembea ndani ya Huduma yako.

Kila mmoja wetu katika huduma ana ushuhuda binafsi juu ya Nguvu za Mungu kwenye maisha yetu. Yesu alijionyesha kwangu wakati sikua na hata wazo la Mungu akilini mwangu. Nilikuwa nimeingia tu kwenye sherehe na nilikuwa tayari kuanza kufurahia wakati huo mzuri. Nilikuwa nimesachukua kinywaji cha kwanza na nipo tayari kunywa, na nikahisi kama nipo ndani ya povu. Sikuweza kusikia chohote. Niliona Bendi ikipiga muziki, watu walicheza na kucheka lakini hakukuwa na sauti. (Hili lilitokea ghafla, na kwa muda usiofahamika). Kisha nikahisi upepo na radi, Nilihisi sauti ya Bwana ikiniingia mwili mzima. Alisema, "Dhambi zilizo rohoni mwako zitakupeleka Kuzimu." Wakati huo, Mungu alifungua ufahamu wangu juu ya dhambi na hukumu. Tofauti na nilivyofundishwa kwenye utamudi wa Kikatoliki, Mungu hapangi dhambi

kwa mafungu. Dhambi zote zilikuwa zikipeleka roho yangu Kuzimu. Nilitupa kinywaji changu na kukimbia. (Sikufikiria kuhusu watu walionizunguka au namna walivyofikiria kunihusu, hofu ya hukumu ya milele iliniingia rohoni.) Mwisho wa barabara nilipiga magoti na kuomba kwa sauti "Mungu nisaidie!" Sikuwahi kusikia toba na sikujuu nifanye nini, nilitafuta msaada usiku ule, hata nikazungumza na mtu anayesoma chuo cha Biblia. Nilienda nyumbani kwake bila ya ye ye kujua kilichonipeleka, alinipa Bangi nivute, nikamjibu hapana, sihitaji. Nikarudi nyumbani. Nilikuwa natafakari "mitaishi maisha ya dhambi na nitakufa na dhambi na sitaweza kufanya lolote kuhusiana na hili"

Kesho yake jioni, rafiki yangu alinialika kwenda naye Hollywood Boulevard (sehemu ambayo sikuwahi kwenda). Tukaenda, Hapa ndipo nilitokutana na watu kutoka Tony and Susan Alamo Christian Ministry. Nilimbiwa jambo moja na mmoja wao, kuwa ni rahisi kumtumikia Bwana. Na kuwa ninachotakiwa kufanya ni kuweka macho yangu kwa Yesu na kutoyatoa kwake. Hayo maneno yaliniingia moyoni kama mshale, na Bwana alinifungua macho kuhusu kumtumikia. Makanisa yote ambayo niliwahi kuudhuria yali-

kuwa yameua imani iliyokuwa moyoni mwangu. Sasa moyo wangu ulijazwa na imani. Nilienda kwenye ibada Canyon Country, Kalifornia, na mwisho wa ibada, nilimwomba Yesu aingie moyoni mwangu. Nilihisi Yesu akiniosha dhambi zote. Nilihisi kama ile damu ya dhambi ya kale ilivurutwa na kutolewa ndani ya mwili wangu na mto wa damu mpya safi ukajia. Nilijua nimebadilishwa. Huu ulikuwa mwanzo wangu mpya na nilitaka kuhusisha wengine hapo hapo.

Baba yangu alikuwa mlevi mwenye roho mbaya ambaye hangeweza kupata ukombozi. Alikuja kanisani akatubu dhambi zake zote na papo hapo akawekwa huru kutokana na pombe. Na akaja kwenye Huduma. Wakati Fulani Susan Alamo alimhoji kwenye moja kati ya vipindi vya Televisheni, Susan akamuuliza Baba yangu, "Ungependa kwa wakati wowote watoto wako watoke kwenye Huduma hii?" Baba yangu akajibu, "Mungu aepushe mbali! Hakuna sehemu nyingine kama Huduma ya Tony na Susan Alamo." Nakubali hakuna sehemu nyingine kama Tony Alamo Christian Ministry.

Shetani ameshindwa, na tumeshinda, tukibeba juu bango la Bwana. Tunakupenda Mchungaji Tony!

Dada Anna Moan

Oklahoma

Kwa Mchungaji Tony,

Niliposikia ujumbe wako kutoka kwa Bwana kuhusu "Matuta chanagarawe," Nilikumbuka ndoto niliyoota nikiwa Dyer, AR, takribani miaka the-lathini iliypita.

Nilikuwa nikitembea juu ya ukuta mwembamba sana; Nikiwa katikati nilianza kupepesuka. Nilikosa nguvu thabiti na kuanguka. Nikaanguka kwenye changarawe na kuanza kuzama haraka sana. Na nikagundua ulikuwa mchanga didimizi.

Kulikuwa na ndugu wawili pale, lakini hawakuweza kunisaidia. Nilizama

hadi mdomoni, kisha nikakuona ukija, Mchungaji Alamo, kama umbali wa futi mia moja. Ulikua ukitembea kwa ukakamavu na kwenye kona ya jicho lako, uliniona na kuja haraka, ukatoa mkono wako na kama 1-2-3 ukaniyuta.

Bwana alinionyesha una nguvu kuitia Roho Wake. Alinionyesha nikiwa kwenye ukuta mwembamba na ulionyooka, lakini sikuweza kuuthibiti mwendo wangu, hivyo nikaanguka. Kama ujumbe wako ulivyo sema, nilikuwa kwenye mchanga didimizi, ni Mungu kuitia kwako alinitoa. Hakuna ambaye angeweza.

Namshukuru Mungu kwa ujumbe wako, kujali kwako, na utii wa hali ya juu wa Mungu.

Tommy Scarcello

Moffett, OK



HUDUMA ZA ALAMO MTANDAONI

www.alamoministries.com



Mchungaji Amos Andala akisambaza majarida ya Alamo na vitabu vya Masihi katika vijiji vya Kenya, Africa.

Zimbabwe

Ndugu Mchungaji Alamo,

Kipindi chako cha huduma za Tony Alamo, kinanibariki kila ninaposikiliza kupitia Radio Africa Two. Kwa mara ya kwanza nilikifahamu kipindi hiki mwezi mmoja uliopita. Ujumbe wake unaelezea vizuri Neno la Mungu kuliko ujumbe mwengine niliowahi kusikia, kwa hiyo nasikiliza kipindi hiki mara kwa mara sasa.

Nashukuru kwa kipindi, na endelea na kazi nzuri.

Wakov

R.N. Gokwe, Zimbabwe, Africa

Ghana

Ndugu Mchungaji Tony,

Mungu aliye juu zaidi, ambaye Mwanawe Yesu Kristo ni mwokozi wetu, akubariki sana kwa kufikisha ujumbe wako unaoshawishi na kuon-goa roho ulionifikia. Na akuwezeshe uongeze eneo lako na kazi na ushawishi.

Inashangaza jinsi uchafu wangu ulivyofunikwa na kubadilishwa kuwa uzuri tangu nilipogundua ujumbe wako. Nilizungukwa na madoa mabaya ya dhambi, lakini kupitia Kristo, ambaye nilikuja kumfahamu, najua dhambi zangu zimesafishwa.

Niliweza kuhusisha familia yangu na marafiki katika zawadi nzuri ya ujumbe kutoka kwenye huduma yako. Kila roho iliyosoma ilishangazwa. Tungefurahishwa sana kama ungetutumia vitu vingi zaidi ambavyo vita-kuwa Baraka, vitu kama majarida, Biblia na vitabu vya Masihi, ili kuongeza ufahamu wetu na ukweli, ili tusije tu-karudia matendo ya kiovu, hivyo basi nasi tutawafundisha wengine waingie katika raha ya mbingu na Mwokozi wetu Yesu siku atakapokuja kutuchukua. Pia tungependa kusikia sauti yako

nzuri, hivyo tungeomba pia ujumbe wako kwenye CD, tunatumaini uta-fanya hivyo katika jina la Yesu.

Tunakushukuru kwa kutupatia ramani sahihi kwa kutuelekeza. Na tutaonyesha shukrani zetu kwa kuhusisha kondoo wengine waliopotea katika ujumbe na majarida.

Wako Mtiifu

N.S. Ashanti, Ghana, Africa

Ndugu Mchungaji Tony Alamo,

Nafurahi kukuandikia barua hii. Kwanza kabisa, hujambo? Natumaini kwa neema za Mungu mweza, u mzima. Nakushukuru kwa kuchukua muda wako muhimu kusoma barua yangu kwa sababu najua wewe ni mtu wa Mungu mwenye mambo mengi.

Nimeokoka hivi karibuni baada ya kusoma ujumbe wako na majarida. Umenibadilisha na kunifanya nitubu kwa namna unavyofundisha Neno la Mungu.

Nataka kujua na kusoma Biblia mwenyewe, lakini kwa sababu ni mwanafunzi, siwezi kumudu bei ya

kununua Biblia, na huku Ghana Biblia inauzwa ghali sana. Nitafurahi sana kama utanitumia Biblia kwa ajili ya matumizi yangu. Ningependa kumaliza kwa maneno haya. Ah-sante.

Rafiki yako,

A.A. Sefwi, Ghana, Africa

Ndugu mpendwa katika Kristo,

Ninakuandikia kutoka Ghana nikitaka kukushukuru wewe na Huduma yako. Mungu awabiriki sana. Nimeokoka kupitia ujumbe wako wenye Kichwa "Hivyo ndivyo Ilivyo." sasa nimemkubali Bwana yesu kama Bwana na Mwokozi.

Mchungaji, Ningependa unitumie nakala hamsini za ujumbe wako. Niko tayari kuwashirikisha marafiki zangu katika Neno la Mungu. Ningependa pia unitumie CD pamoja na vitu vingine vitakavyoniwezesha kulisoma vizuri Neno la Mungu.

Bwana Yesu Kristo akubariki sana. Amen.

A.E. Ghana, Africa

ASKARI WA JANGWANI

(Inaendelea kutoka ukurasa wa 4)

hii?" Upo hapo kwa sababu MUNGU anamuandaa mwanamume au mwanamke kupeleka ujumbe wa wokovu, upendo, huruma isiyo na mwisho na neema kwa wanadamu. MUNGU atakulinda na utakubali uzoefu huu wa jangwa. Na utamshukuru MUNGU kwa jambo hilo. Wakati mzuri ambaa utawahi kupata ni pale MUNGU anaposhuka chini jangwani, na hapo mbele yako kuna kichaka kinachochomeka, katika ile sehemu ya upweke. Wakati ukiwa na hamu ya kurdii nyumbani, na mwenye uchovu, ghafla MALAIKA wa MUNGU anatokea na unaanza kumshukuru MUNGU kwa mlima wa upweke unaopigwa na upepo. Kisha atakuongoza katika ROHO WAKE kugusa nyoyo za watu, waume kwa wake kwa ukombozi WAKE mkuu wa kiungu.

Anza sasa kwa kusali hii sala kwa MUNGU.

BWANA wangu na MUNGU wangu, ihurumie roho yangu, mimi mwenye dhambi³³ ninaamini kwamba YESU KRISTO ni mwana wa MUNGU aliye hai.³⁴ Ninaamini kwamba alikuifa msalabani na kumwaga damu yake ya thamani ili nisamehewe dhambi

zangu zote nilizozifanya hapo awali.³⁵ Ninaamini kwamba Mungu alimfufua YESU kutoka kwa wafu kupidia nguvu za ROHO MTAKATIFU³⁶ na ya kuwa ameketi upande wa kuume wa MUNGU kwa wakati huu akisikiliza maungamo ya dhambi zangu na maombi yangu haya.³⁷ Ninafungua mlango wa moyo wangu na kukukaribisha moyoni mwangu, BWANA YESU.³⁸ Nioshe dhambi zangu kwa damu uliyoimwaga kwa ajili ya nafsi yangu pale msalabani Kalivari,³⁹ hutanikataa, BWANA YESU, utanisamehe dhambi zangu na kuiokoa roho yangu. Ninalijua hili kwa sababu NENO LAKO, yaani Biblia linasema hivyo.⁴⁰ NENO LAKO linasema hutamkataa yejote na mimi nikiwemo.⁴¹ Hivyo ninajua kwamba umenisikia, na ya kuwa umenijibu; na ninafahamu kwamba nimeokoka.⁴² Ninakushukuru BWANA YESU kwa kuokoa roho yangu na nitaonesha shukrani zangu kwa kfanya yale unayoniamuru na kwa kutoenda dhambi tena.⁴³

Baada ya kuokoka YESU alisema ni lazima kubatizwa kwa kuzamishwa kabisa kwenye maji mengi kwa jina la BABA, MWANA na ROHO MTAKATIFU.⁴⁴ Kwa makini soma Biblia ya KJV, tafsiri ya Kiswahili ya The Bible League, Waenezaji wa Neno la Mungu tangu 1938 na ufanye inavyosema.⁴⁵

BWANA anakutaka uwaambie wen-gine kuhusu wokovu wako. Unaweza kusambaza makala ya Injili ya mchungaji Tony Alamo. Tutakutumia makala hizi bila malipo. Tupigie simu ama ututumie barua pepe kwa habari zaidi. Mshirikishe na mtu mwingine ujumbe huu.

Iapo unataka dunia yote iokolewa, kama YESU anavyoamuru, basi usimwibie MUNGU zaka na sadaka zake. MUNGU alisema, "Je! Mwanadamu atamwibia Mungu? Lakini ninyi mnaniibia mimi. Lakini ninyi mwasema, Tumekuibia kwa namna gani? Mmeniibia zaka na dhabihu. Ninyi mmelaaniwa kwa laana; maana mnaniibia mimi, naam, taifa hili lote [na dunia hii yote]. Leteni zaka [zaka ni asilimia 10 ya mapato yako yote] kamili ghalani, ili kiwemo chakula [chakula cha kiroho] katika nyumba yangu [roho zilizookolewa], mkanijaribu kwa njia hiyo, asema Bwana wa majeshi; mjue kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha, au la. Nami kwa ajili yenu nitamkemea yeze alaye, wala hataharibu mazao ya ardhi yenu; wala mzabibu wenu hautapukutisha matunda yake kabla ya wakati wake katika mashamba, asema Bwana wa majeshi. Na mataifa yote watawaiteni heri; maana mtakuwa nchi ya kupendeza sana, asema Bwana wa majeshi" (Malaki 3:8-12).

³³ Zab. 51:5; Rum. 3:10-12, 23 ³⁴ Mat. 26:63-64; 27:54; Lk. 1:30-33; Yoh. 9:35-37; Rum. 1:3-4 ³⁵ Mdo. 4:12; 20:28; Rum. 3:25; 1 Yoh. 1:7; Ufu. 5:9 ³⁶ Zab. 16:9-10; Mat. 28:5-7; Mk. 16:9, 12, 14, Yoh. 2:19, 21; 10:17-18; 11:25; Mdo. 2:24, 3:15; Rum. 8:11; 1 Kor. 15:3-7 ³⁷ Lk. 22:69; Mdo. 2:25-36; Ebr. 10:12-13 ³⁸ 1 Kor. 3:16; Ufu. 3:20 ³⁹ Efe. 2:13-22; Ebr. 9:22; 13:12, 20-21; 1 Yoh. 1:7; Ufu. 1:5, 7:14 ⁴⁰ Mat. 26:28; Mdo. 2:21; 4:12; Efe. 1:7; Kol. 1:14 ⁴¹ Mat. 21:22; Yoh. 6:35, 37-40; Rum. 10:13 ⁴² Ebr. 11:6 ⁴³ Yoh. 5:14, 8:11; Rum. 6:4; 1 Kor. 15:10; Ufu. 7:14; 22:14 ⁴⁴ Mat. 28:18-20; Yoh. 3:5; Mdo. 2:38; 19:3-5 ⁴⁵ Kumb. 4:29; 13:4; 26:16; Yos. 1:8; 22:5; 2 Tim. 2:15; 3:14-17; Yak. 1:22-25; Ufu. 3:18

Tafadhali wasiliana nasi kwa habari zaidi au kwa vitabu vyetu vyenye mada nyingine ambazo unaweza kuvutiwa nazo:

**Tony Alamo, World Pastor, Tony Alamo Christian Ministries Worldwide • P.O. Box 2948, Hollywood, CA 90078
Namba yetu ya simu kwa ajili ya maombi na habari iliyo wazi kwa saa ishirini na nne ni: (661) 252-5686 • Faksi: (661) 252-4362**

www.alamoministries.com • info@alamoministries.com

Huduma ya Tony Alamo Christian Ministries Worldwide hutoa mahali pa kuishi pamoja na vitu vyote muhimu kwa maisha kwa wale walio Marekani ambaa wanataka kumtumikia BWANA kwa miyo yao yote, roho zao zote na nguvu zao zote.

**Huduma yetu hufanyika jijini New York kila Jumanne, saa mbili usiku na mahali pengine kila usiku.
Tafadhali wasiliana nasi kupidia simu namba (908) 937-5723 kwa habari zaidi. CHAKULA HUTOLEWA BAADA YA KILA IBADA.**

**Tuma maombi ujipatie kitabu cha Mchungaji Alamo kitiwacho, The Messiah, kinachomwonesha KRISTO
alivyo katika Agano la Kale kwa jumbe za unabii zipatazo 333.**

Kuwa mmoja wa watumishi katika kuvuna roho za watu kwa kuwa msambazaji wa makala na vitabu vya Mchungaji Alamo Machapisho yetu na jumbe kwenye tepu za sauti hayalipishwi kitu ikiwemo gharama ya kusafirisha kupidia meli.

Iwapo kuna mtu atajaribu kukulipisha, tafadhali tupigie simu kwa namba: (661) 252-5686.

**MAKALA HIZI ZIMEBEBA MPANGO WA KWELI WA UKOMBOZI (Matendo ya Mitume 4:12)
USIZITUPE: ZIFIKISHE KWA MTU MWINGINE.**

**Kwa wale ambaa mko kwenye nchi nyingine, tunawashauri kutafsiri makala hizi kwa lugha zenu. Iwapo
mtachapisha tena, tafadhali jumuisha haki hii na usajili:**